GRPS my choice®
Grand Rapids Public Schools

MWONGOZO WA COVID-19

Ndugu Mzazi/Mlezi,

Tunafurahia kukupatia Mwongozo wetu wa COVID-19 wa GRPS.

Mwongozo huu unanuiwa kama mwongozo wa marejeleo ya upesi kwa wazazi na walezi wote wa GRPS kila tunavyoendelea kupitia maradhi tandavu ya COVID-19.

Huu ni waraka huishi utakaosasishwa kila mabadiliko au maelezo mapya yanapoibuka.

Ikiwa una maswali au unataka maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na shule yako.

Kwa dhati,

Leadriane Roby, Ph.D.
Msimamizi wa Shule

02 Dashibodi ya Data ya COVID-19

03 Kikagua Afya cha Kila Siku cha Afya ya Wanafunzi

04 Kumbusho la Dalili kwa Wanafunzi

05 Cha Kufanya ikiwa Waajiriwa Wana Matokeo Chanya/ Mwingiliano wa Karibu

06 Sampuli ya Notisi ya Wazazi ya Kisa Chanya

07 Chati Tiririshi ya Wilaya ya Mbinu za Kushughulikia Barakoa

08 Vidokezo na Taratibu za Kusafisha

09 Huduma za Lishe

10 Kumbusho la Teknolojia

11 Usafiri

12 Kusasisha Maelezo ya Mwasiliani

GRPS my choice®
Grand Rapids Public Schools

COVID-19
DASHIBODI YA TAKWIMU

Ili Kufahamisha Kurudi Kwetu kwenye Shule ya Ana kwa Ana

TAKWIMU	SHABAHA	UFAFANUZI WA DARAJA YA HATARI YA SHABAHA	VYANZO VYA DATA
KIASI CHA CHANYA CHA KAUNTI *wastani wa siku 7*	**< 5% HATARI NDOGO** **Zingatia 5-10%**	**VIWANGO VYA HATARI** Chini = <5% Wastani = 5-8% Juu = 8-10% Juu Kabisa = >10%	Ramani ya Mwanzo Salama ya MI Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent
MATUKIO YA KAUNTI KWA KILA 100,000 *kwenye siku 14*	**LENGA visa 1-5/100K** **Zingatia visa 6-20/100K**	**VISA/100,000:** Chini = <20 Wastani = 21-50 Juu = 51-200 Juu Kabisa = >200	Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent Vigezo & Viashiria vya CDC vya Hatari Shuleni
MATUKIO YA JAMII KWA KILA 100,000 *kwenye siku 14*	**LENGO:** Sawia na au chini ya matukio ya kaunti/100K **ZINGATIA:** juu kuliko matukio ya kaunti/100K	**Zaidi ya visa 100/100K chini kuliko kaunti:** songea chini kwa daraja ya hatari **Ndani ya visa 100/100K vya kaunti:** bakia kwenye daraja sawia ya hatari **Zaidi ya visa 100/100K zaidi kuliko kaunti:** songea juu kwa daraja ya hatari	Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent Hatari ya KCHD ya kiunzi cha usambazaji wa COVID shuleni
MATUKIO YA KAUNTI KWA KILA MILIONI 1 *kwenye siku 7*	**LENGA Chini < 7** **Zingatia A-E**	**VISA/MILIONI 1:** Chini = <7 A = 7-20 B = 20-40 C = 40-70 D = 70-150 E = >150	Ramani ya Mwanzo Salama ya MI
MAELEZO MENGINE *Mwelekeo wa Vipimo Chanya au Visa vya COVID-19*	**UFUATILIZI ENDELEVU** *Hakuna Shabaha Maalum*	• Viwango vya Kulazwa kwa ajili ya COVID-19 • Idadi ya Vifo kwa ajili ya COVID-19 • Mwelekeo wa matukio – *Unaongezeka au unapungua kwenye siku 7 zilizopita zinapolinganishwa na siku 7 kabla yake.* • Nguvu ya Uwezo wa Uangalizi wa Afya • Mikakati Yote ya Kupunguza Hatari Yako Mahali Kwake • Visa chanya vya GRPS vinawasilishwa kwenye shule kwa siku 14	Ramani ya Mwanzo Salama ya MI Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent Vigezo & Viashiria vya CDC vya Hatari Shuleni Dashibodi ya Shule ya COVID-19 ya KISO Maradhi Tandavu Yamefafanuliwa Mahojiano ya Ufuatilizi wa Mwingiliano

Dashibodi ya Data ya COVID-19 ya GRPS itajazwa na data na kusasishwa kila wiki kwenye tovuti ya wilaya. Dashibodi ya Data itatumiwa ili kuongoza uamuzi wa Wilaya yetu kwa kushauriana na Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent.

COVID-19 UKAGUZI WA KILA SIKU WA AFYA YA WANAFUNZI

Kwa mujibu wa mwelekeo kutoka kwa CDC, Idara ya Michigan ya Huduma za Afya na Binadamu, na Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent, Grand Rapids Public Schools itasimamia kikagua afya cha kila siku cha afya ya wanafunzi kwa wanafunzi wanapokuwa shuleni, ana kwa ana.

WANAFUNZI WA PK-5

	Mwandani A	Mwandani B
Tarehe ya Mawasiliano	Jumapili & Jumatatu	Jumatano & Alhamisi
Eneo la Mawasiliano	Baruapepe ya mzazi au ujumbe wa mzazi	Baruapepe ya mzazi au ujumbe wa mzazi

WANAFUNZI WA 6-12

	Mwandani A	Mwandani B
Tarehe ya Mawasiliano	Jumapili & Jumatatu	Jumatano & Alhamisi
Eneo la Mawasiliano	Baruapepe ya mwanafunzi, baruapepe ya mzazi au ujumbe wa mzazi	Baruapepe ya mwanafunzi, baruapepe ya mzazi au ujumbe wa mzazi

Walimu na/au wateuliwa wao wanatarajiwa kuhakiki data ili kuona kama wanafunzi wowote waliowekewa alama ya “Ndio” kwenye swali lolote kati ya maswali yoyote na bado wakahudhuria shule siku hiyo. Ikiwekewa alama ndio, ni lazima mwanafunzi atumwe papo hapo hadi kwenye eneo la kujitenga ili kutathminiwa zaidi. Waajiriwa wa ofisi ya afya watatii taratibu zote za afya zinazohusu COVID ili kung’amua kama mwanafunzi anafaa kutumwa nyumbani au kurudi darasani.

Waajiriwa wote wataambiwa wawe waangalifu kuhusu kutambua wanafunzi wanaoonekana kuwa wana dalili za COVID-19 wanapokuwa shuleni. Ikiwa mwanafunzi ana dalili zinazoonekana, ni lazima mwanafunzi huyo atengwe papo hapo na wanafunzi wengine na waajiriwa wa ofisi ya afya ni lazima waarifiwe papo hapo. Waajiriwa wa ofisi ya afya watang’amua kama mwanafunzi anafaa kurudishwa nyumbani.

Waajiriwa wa ofisi ya afya watatoa miongozo ya kujitenga na karantini kwa wanafunzi, wazazi, au walezi na kwa waajiriwa mwafaka wa shule kwa mujibu wa Zana ya Shule ya KCHD. Hii itahakikisha usahihi na uwianifu.

Ikiwa mwanafunzi alihudhuria siku zote mbili za ana kwa ana na alishindwa kukamilisha kikagua afya cha kila siku, mawasiliano yatatumwa kupitia baruapepe, simu ya roboti, na ujumbe wa maandishi hadi kwa wanafunzi/wazazi mnamo Jumatano kwa Mwandani A na Jumapili kwa Mwandani B.

COVID-19 KUMBUSHO LA DALILI KWA WANAFUNZI

Kabla ya kuondoka shuleni, tafadhali angalia kama mwanafunzi uliye naye ana dalili za COVID-19.

Mbakishe mtoto wako nyumbani ikiwa anapitia yoyote kati ya dalili zifuatazo:

- Homa ya 100.4F au zaidi AU mwili umekuwa moto
- Kikohozi kipya au badiliko kwenye kikohozi
- Kuhema
- Upotezaji mpya wa ladha na harufu
- Kuwashwa koo
- Maumivu mwilini
- Kuendesha, kutapika, au kichefuchefu
- Kuumwa kichwa sana
- Uchovu mno
- Pua kuzibika au kuvuja kamasi

Pia mbakishe mtoto wako nyumbani ikiwa:

- Umekuwa na mwingiliano wa karibu au unaishi na mtu aliyepimwa na kupata matokeo chanya ya COVID-19
- Mwanafunzi au mwanafamilia yoyote anasubiri matokeo ya kipimo cha COVID 19.
- Au umesafiri nje ya nchi kwenye siku 14 zilizopita

Ikiwa unaamini kuwa dalili za mwanafunzi uliye naye zinahusiana na bainisho mbadala lililo wazi, tafadhali wasiliana na muuguzi wa shule kabla ya kumpeleka mtoto wako shuleni. Huenda ikakubidi utoe ithibati ya bainisho hili.

Mtoto wako akianza kupata yoyote kati ya dalili hizi wakati wa siku ya shule, shule itamtenga mtoto wako mbali na wengine na itakupigia simu ili kupanga umchukue. Ikiwa hatukuweza kuwasiliana na wewe, tutawapigia simu wawasiliani wa dharura walioorodheshwa ndani ya Synergy. Ni muhimu sana uendelee kusasisha maelezo yako ya mwasiliani ndani ya Synergy. Hatutoweza kumrudisha nyumbani kwa basi mwanafunzi uliye naye ikiwa ana dalili za COVID-19.

Kutakuwepo nyakati ambapo ni lazima kwa wanafamilia (k.v. ndugu) kubakia nyumbani pia. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi maamuzi haya yanavyofanywa, tafadhali rejelea Mwongozo wa Kaunti ya Kent kwa Shule hapo www.accesskent.com/Health/CommDisease/pdfs/K-12-COVID19-SYMPTOM-TESTING-PROTOCOL.pdf

COVID-19

Cha Kufanya Ikiwa Wanafunzi Wana Matokeo Chanya au Mwingiliano wa Karibu

Wilaya itatii itifaki na mahitaji ya MDHHS/OSHA ikiwa mtu binafsi ana kisa kilichothibitishwa cha COVID-19, ikiwemo mahitaji ya kuripoti na kudumisha rekodi. Wilaya itakusanya maelezo ya mwasiliani ya waingiliani wowote wa karibu wa mtu aliyeathirika kuanzia siku mbili kabla ya kupata dalili hadi wakati ambapo alikuwa shuleni kwa mara ya mwisho.

Ni lazima wanafunzi wote wakamilishe Ukaguzi wa Afya wa Kila Siku wa COVID-19 kabla ya kuingia shuleni (Tazama Ukurasa wa 04).

Ukijibu ndio kwenye swali lolote kati ya maswali kwenye Ukaguzi wa Afya wa Kila Siku wa COVID-19, ni lazima:

01 Ubakie nyumbani

02 Uarifu shule yako

Ukija shuleni na ukianza kupata dalili kwenye siku ya shule, ni lazima:

01 Uarifu mwalimu/muuguzi wako wa shule

02 Uondoke shuleni papo hapo

Ukipata matokeo chanya au ikiwa umetambuliwa kama mwingiliani wa karibu wa mtu aliyepata matokeo chanya (ndani ya 6’ kwa dakika 15 au zaidi pamoja na au bila barakoa – dakika 15 kwa mtawalia si lazima iwe jumla ya dakika 15 kwa wakati mmoja):

01 Ubakie nyumbani au uondoke shuleni papo hapo.

02 Uwasiliane na muuguzi wako wa shule. Muuguzi wako wa shule atatekeleza ufuatilizi wa mwingiliano na kukupatia miongozo ya karantini/kujitenga.

COVID-19 SAMPULI YA NOTISI YA WAAJIRIWA YA KISA CHANYA

SISAMBAZE

Ndugu Mzazi/Mlezi,

Unapokea barua hii kwa sababu mtoto wako, NAME, ametambuliwa kuwa ni mwingiliani wa karibu kwa mwanafunzi au mwajiriwa kwenye shule yetu na amepimwa na kupata matokeo chanya ya COVID-19. Ofisi yetu ilipata kujua mnamo DATE kipimo kilikuwa chanya. Tuna wajibu wa kutambua wale ambao wanaweza kuchukuliwa kuwa ni waingiliani wa karibu na miongozo ya CDC huku tunailinda faragha ya mwanafunzi uliye naye. Tunaendelea chini ya mwongozo wa Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent. Tafadhali mbakishe mtoto wako nyumbani na subiri mawasiliano kutoka kwa Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent. Ikiwa hujapokea mawasiliano kutoka kwa Idara ya Afya kwenye masaa 48 yafuatayo, tafadhali wasiliana na ofisi yetu.

Mikakati yote imechukuliwa ili kulinda uzima wa mtoto wako, ikiwemo kusafisha na kutakasa jengo vizuri. Tafadhali mfuatilie mtoto wako ili kuchunguza kuanza kwa dalili zinazohusu COVID-19. Ukiona badiliko lolote kwenye afya ya mtoto wako, tafadhali mpigie simu mtoa huduma wako wako wa kawaida wa kimatibabu.

Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali wasiliana na muuguzi wako wa shule – INSERT CONTACT INFORMATION

Dalili za COVID-19:

- Kikohozi
- Kuumwa kichwa
- Homa (ya 100.4 au zaidi)
- Kuwashwa Koo
- Maumivu kwenye Misuli
- Kichefuchefu au kutapika
- Kibaridi
- Upotezaji mpya wa ladha na harufu

Nyenzo za kupata vipimo na uangalizi wa afya:

- Wasiliana mtoa huduma wako wa kimatibabu ili kuagiza na kuratibu vipimo
- Wasiliana na Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent kwa nambari (616) 632-7100
- Pigia simu nambari ya dharura ya COVID ya Michigan kwa nambari (888) 535-6136
- www.michigan.gov/coronavirus

Ikiwa mwanafunzi uliye naye anaanza kupata dalili au anasubiri kipimo cha COVID:

Ni lazima mwanafunzi uliye naye abakie nyumbani. Ni lazima wanafamilia wote wabakie nyumbani na wawekwe kwenye karantini kwa siku 14. WANAFUNZI NA WANAFAMILIA HAWARUHUSIWI KUHUDHURIA SHUGHULI ZOZOTE SHULENI MPAKA WAPEWE IDHINI NA IDARA YA AFYA YA KAUNTI YA KENT.

Kwa dhati,

Jina la Kwanza Jina la Mwisho
Mwalimu Mkuu

COVID-19 MCHAKATO WA BARAKOA

Wilaya, kwa kutii Miongozo ya Jimbo la Michigan na CDC, imeanzisha mpango wa kurudi kwenye mafunzo unaojumuisha matarajio ya wanafunzi kuvaa barakoa shuleni kwa usalama wao wenyewe, wa wengine, na wa jamii kwa jumla. Ikiwa mwanafunzi hawezi kuhimili barakoa kwa ajili ya matatizo ya afya yaliyorekodiwa na daktari, inapendekezwa sana azingatie ukufunzi pepe kwa sababu hali yake ya afya inamweka yeye na wengine kwenye kategoria ya hatari kubwa. Kunapotokea tukio ambapo licha ya hali ya afya iliyorekodiwa, mzazi anachagua ukufunzi wa mseto/ana kwa ana, wilaya itachukua hatua zifuatazo ili kujaribu kulishughulikia ombi hili kimantiki.

Mbinu za kushughulikia huenda zikajumuisha, lakini haziwekewi kikomo kwa:

- Kinga
- Mseto wa mitindo/Aina za Barakoa
- Vigawanya Akrikiliki
- Ratiba
- Fursa za Mara kwa Mara
- Vivutio
- Fursa za Breki Zilizoratibiwa
- Kutengana Kijamii Kulikoongezwa
- Mazingira Mbadala

* **Mafunzo ya mbali huenda yakahitajika ikiwa hakuna yoyote kati ya mbinu za kushughulikia iliyofaulu.**

CHATI TIRIRISHI YA WILAYA YA MBINU ZA KUSHUGHULIKIA BARAKOA

MZAZI ANAWASILISHA OMBI LA UDHURU WA KUVAA BARAKOA

Mwanafunzi ana Hali Iliyopo Iliyorekodiwa na Daktari ambayo Inakidhi Kigezo cha Uzingativu cha Mpango wa Afya, Mpango wa 504, au IEP

NDIO

- Hakiki Data na Anzisha Msingi wa Uhimilifu
- Hakiki Data na Tambua Udhuru/ Nyudhuru za Kimantiki ili Kujenga Uhimilifu wa Wanafunzi na FUNZA Kuvaa Barakoa
- Hakiki Data Kila Wiki ya Uhimilifu Unaoongezeka kwenye Mazingira Tofauti
- Tekeleza Udhuru/Nyudhuru
- Hakiki Data kwenye Wiki ya 3 ili Kung'amua Mapendekezo ya Ziada
  Kujumuisha pendekezo huenda kukasababisha mwanafunzi arudi kwenye ukufunzi pepe ikiwa hakuna mwendeleo au mwendeleo kidogo umetokea.

LA

- Fahamisha Mzazi kuhusu Haja ya Kurekodi Hali ya Afya
- Hati Ikipokewa/Inapopokewa, Fuata Mchakato wa Wilaya wa Uzingativu (Mpango wa Afya, Mpango wa Kifungu cha 504, IEP)

MSAIDIZI:

Furushi la Zana la AccessKent– www.accesskent.com/Health/CommDisease/pdfs/SchoolChildcareToolkit.pdf

COVID-19
VIDOKEZO NA MAKUMBUSHO YA MAFUNZO

UFAFANUZI

Kusafisha kunaondoa vidudu, uchafu, na kasoro kwenye sehemu au vitu kwa kutumia sabuni na maji. Mchakato huu si lazima uangamize vidudu vyote lakini unapunguza hatari ya kusambaza uambukizo.

Kutoharisha kunapunguza idadi ya vidudu kwenye sehemu au kitu hadi kwenye kwiango kinachokubalika, kulingana na vigezo vya afya vya umma, na kunafanya kazi kwenye vitu ili kupunguza hatari ya kusambaza uambukizo.

Kutakasa kunaua vidudu au vitu kwa kutumia kemikali lakini si lazima isafishe sehemu chafu. Inapendekezwa usafishe sehemu na vitu kwa kutumia sabuni na maji kabla ya kuvitakasa.

Tunaipatia kipaumbele afya ya wanafunzi na waajiriwa.

Kuvaa barakoa, kuosha mikono yako na kutekeleza kutengana kijamii kadiri ya uwezo wa watu kutakuwa muhimu sana ili kupata mwaka salama wa shule.

Kusafisha kunapunguza hatari ya kusambaza uambukizo kwa kuondoa na kuua vidudu kwenye sehemu zinazoguswa sana na watu. Shule ya mtoto wako inatayarishwa kuhusiana na itifaki za utunzi.

Bidhaa za usafishaji zinazokidhi vigezo vinavyopendekezwa vya CDC, EPA, na sera za wilaya.

- Shule zinasafishwa kila usiku.
- Shule za siku 2 kwa wiki (baina ya wandani mseto) zinasafishwa kwa kina.
- Sehemu za kuguswa zinatakaswa na kusafishwa siku nzima.
- Matumizi yenye kikomo ya vitu vinavyoshirikiwa yanatekelezwa.
- Sehemu jumuishi na mabafu yanayoshirikiwa yanasafishwa mara nyingi kwenye siku ya shule.

COVID-19 SASISHO LA HUDUMA ZA LISHE

Milo ya Vyakula vya Shule / Milo ya Vyakula vya Kubeba na Kuenda

CHAKULA CHA MCHANA NA KIAMSHAKINYWA CHA SHULE YA ANA KWA ANA:

Tutatoa chakula cha mchana na kiamshakinywa shuleni wakati wa siku zilizoratibiwa za mseto wa ana kwa ana kwa Wandani A na B. Milo ya vyakula itakuwepo kwenye mkahawa.

MILO YA VYAKULA VYA KUBEBA NA KUENDA:

Shule zinapotoa ukufunzi wa mseto wa ana kwa ana, vituo vya milo ya vyakula vya kubeba na kuenda vitakuwa Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia 12:30 p.m. hadi 1:30 p.m. Kwenye kila shule ndani ya wilaya kwa wanafunzi pepe. Mwanafunzi wowote aliyeandikishwa kwenye GRPS anaweza kupokea mlo wa chakula kwenye eneo lolote kati ya maeneo yetu.

COVID-19 KUMBUSHO LA TEKNOLOJIA

Ndugu Mzazi/Mlezi,

Tunakuandikia barua ili kushiriki maelezo yaliyosasishwa kuhusu usambazaji na ukarabati wa vifaa vya teknolojia.

Kama kumbusho, kabla ya kuanza kwa shule mnamo Agosti, tulitangaza kuwa wilaya inatoa vifaa vya teknolojia vya kimoja kwa mmoja kwa wanafunzi WOTE (iPad kwa madarasa ya PK-1 na Chromebook kwa madarasa ya 2-12).

Wakati mafunzo ya ana kwa ana yanapopatikana, wanafunzi watatarajiwa watumie na walete vifaa vyao vinavyotolewa na wilaya kwenye mafunzo ya ana kwa ana. Tunawahimiza wazazi wote tafadhali wahakikishe wanatenga muda wa kuchukua kifaa cha mwanafunzi waliye naye.

Pia tunajitolea kufanya kazi na familia ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaweza kufikia huduma imara ya Intaneti (mitandao-hewa ya pasiwaya au Comcast Internet Essentials inayogharimiwa na mfadhili).

Tafadhali ratibu miadi kwa kupiga simu kwa nambari (616) 301-1111:

- Ikiwa unahitaji kuchukua kifaa cha mwanafunzi uliye naye
- Ikiwa unahitaji usaidizi na ufikiaji wa intaneti
- Ikiwa unahitaji ukarabati kwenye kifaa cha mwanafunzi uliye naye

Siku na masaa ya huduma za Kituo cha Huduma ya Teknolojia ni:

- Jumanne kuanzia 9:00 AM to Saa Sita Mchana.
- Alhamisi kuanzia 1:00 p.m. hadi 6:00 p.m.

Kituo cha Huduma ya Teknolojia kiko hapo Franklin Campus Early Childhood Center (1326 Thomas St. SE, Grand Rapids, MI 49506).

Asante tena kwa subira, ufahamu, na usaidizi unaoendelea kutupatia.

Kwa dhati,

Leadriane Roby, Ph.D.
Msimamizi wa Shule

COVID-19 SASISHO LA USAFIRI BASINI

NAMBARI MPYA YA DHARURA YA USAFIRI
(616) 819-6100

MIONGOZO YA AFYA NA USALAMA YA USAFIRI WA BASI MANJANO:

- Mabarakoa yanahitajika
- Viti vilivyoteuliwa vinahitajika
- Madereva watakamilisha chati za viti kabla ya siku ya kwanza ya shule ya ana kwa ana
- Viti viwili vya kwanza kwenye pande zote mbili za basi vitabakia
- Mahitaji ya kutengana kijamii
- Ndugu wanaweza kukaa pamoja

COVID-19 SASISHO LA MAELEZO YA MWASILIANI

Ndugu Mzazi/Mlezi,

Kwa ajili ya uamuzi na hali zinazozidi kubadilika kuhusiana na COVID na shule zetu, ni muhimu sana kwa wilaya na shule kuwa na idhini na maelezo ya mwasiliani ya hivi karibuni ya wazazi na walezi.

Ni lazima wazazi na walezi watoe idhini ili wilaya na shule zitume baruapepe, simu za mashine, na ujumbe wa maandishi. Wazazi na walezi wana ufikiaji wa fomu ya idhini kupitia akaunti yako ya ParentVue. Utahitaji nambari ya mwanafunzi ya mtoto wako ili kukamilisha fomu ya idhini, ambayo pia inapatikana kwenye ParentVue.

Tunawahimiza wazazi na walezi wote wachague kujisajili ili kupokea mojawapo au zaidi ya mawasiliano hayo.

Bofya hapa ili kukamilisha fomu ya idhini.

Pia tunawahimiza wazazi na walezi wapende kurasa binafsi za Facebook za shule na wilaya na wafuatilie tovuti ya wilaya hapo grps.org ili kupata maelezo na habari muhimu.

Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi uliye naye. Asante!

Kwa dhati,

Leadriane Roby, Ph.D.
Msimamizi wa Shule